

**KENDJET -2012**  
**FASIHI 102/3**  
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SWALI LA 1**

- a).Mwandishi anakejeli umma/jamii ambayo haitambui bidii ya mkulima (alm2)
- b) (i). Tarbia – Mishororo minne kila ubeti  
(ii) Mathnawi – Vipande viwili / mgao miwili  
(iii) Mtiririko – Vina vya kati na mwisho vinatiririka. Zozote mbili (2 x 2 =4)
- C (i). Takriri – Neno mkulima kurudiwa / kukaririwa.  
(ii) Tashbihi – Mkono wa mkulima ni mgumu kama chuma  
(iii) Taswira – Picha ya namna mgongo wa mkulima ulivyoinama.  
(iv). Chuku – Mkono ulivyo mgumu kama chuma  
(v). Nidaa – Hata dawa wamnyima!  
(vi) Balagha – Nani atakayepuma?
- d). Maisha ya mkulima ni ya taabu na husikitisha, makao yake ni ya duni naye amedhoofika kimwili ilhali huyu mkulima ndiye mtu muhimu katika maisha. (alm4)
- e). (i) Anadharauliwa  
(ii) Akijiingiza/ Akijitia  
(iii) Atakayeishi  
(iv) Heshima (Zozote 4 x 1 = 4)

**SWALI LA 2**

- a). (i) Anayezungumza ni Shehe Kijuba  
(ii) Anaongea na Salim  
(iii) Walikuwa kwa Shehe Kijuba  
(iv) Salim alikuwa amekuwa kwa Shehe Kijuba kutafuta kazi yakufunza dini msikitini. (alm4)
- b). Salim alikaribishwa kwa:  
(i) Alipata kazi ya kufunza dini hapo Msikitini  
(ii) Alipewa chumba cha kulala chenye choo na bafu  
(iii) Alipewa redio kaseti  
(iv) Alikabidhiwa pesa za nauli ya usafiri alizodai za kwenda kuvunia viazi na maharagwe kwao Shehe Kijuba  
(v) Shehe kupata wakati wa kuendesha shughuli zake za kucheza bao  
(vi) kuongeza mapato yake kutokana na sadaka kemkem (zozote 6 x 2 = 12)
- c)(i) Shehe Kijuba kupoteza pesa zake kutokana na kulaghaiwa na Salim kuhusu viazi na maharagwe.  
(ii) Vijana wa pale mtaani kupoteza pesa zao kwa ulaghai kuwa wangenunuliwa vifaa vya kuchezea mpira  
(iii) Mfuko wa Shehe ulienda  
(iv) Kaseti pia ilibebwa  
(v) Shehe Kijuba kubakia kwa majuto na fedheha kubwa. (zozote 4 x 1 = 4)

**SWALI LA 3**

Hadithi fupi

Mwanamke anaendeleza mateso/dhuluma dhidi ya mwanamke mwenzake kwa njia zifuatazo:

- (i). Kazi – Mtoto wa kike anafanyishwa kazi nyingi za nyumbani na kutarajiwa asome kwa wakati huo huo bila utetezi wowote kutoka kwa wanawake (mama Zena)
- (ii). Ndoa – Wanawake hawakuwa wakisomeshwa sana na hata wangeliozwa mara tu pangetokea mume wa kuwashika mkono.
- (iii) Zena anamweleza mamake kuhusu makuruhu aliyotendewa na mumewe badala yake analaumiwa kwa kutotimiza wajibu wake hakutoa, suluhisho mwafaka.

- (iv) Dhuluma ndoani zinapozidi hadi kufikia kipigo, Zena anashindwa kumweleza mamake nu hivyo kuendelea kuteseka hadi mwisho anashindwa kuhimili.
- (v) Wazazi wa Ali akiweko mamake Ali hawakufanya lolote kuzuia madhara yaliyompata Zena ndani ya ndoa. Ali alikuwa kama mfalme kwa mamaye.
- (vi) Zena anapomshauri mamake kuhusu swala la kujiingiza siasani, mamake anamkashifu .
- (vii) .Wakati wa kampeni za kisiasa baadhi ya wanawake walichangia katika kumsengenya na kupaka jina lake tope/ walimwita Malaya. (zozote 6 x 2 = 12)

- (i). Naseko anaposhikwa kwenda kuozwa kwa mume badala ya wanawake walioshuhudia kumsaidia walianza kumsimanga na kumcheka.
- (ii). Mama Naseko alifanamu vyema posa ya Naseko lakini hakufanya lolote kuzuia tukio hilo, hakuwa na sauti.
- (iii). Mkewe Bi Sakaja wa kwanza aliyemzalia mtoto mmoja hakuweza kijitetea dhidi ya dhuluma ndoani kwa kuogopa talaka wake zake wengine nao pia hawakumpinga.
- (iv). Mkewe Sakaja Wa pili kuteseka ndoani hadi kufa bila kuchukua hatua yoyote.
- (v) Wanawake ndio wanaomlaki Naseko kwa mzee Sakaja bila kujali kilio chake. (zozote 4 x 2 = 8)

#### SWALI LA 4

a) i) Ni Bi Farashuu aliyekuwa akizungumza na

ii) Kabi

iii) Ni nyumbani kwa Kabi

iv) Alikuwa akimrejelea Maimuna punde tu alipofika kwa Kabi baada ya safari ndefu.

v) Alitamka haya alipompata Maimuna nyumbani kwa Kabi na kufahamishwa kuwa Maimuna ndiye mke mjukuwe aliyetarajia kumwoa (alama 1 x 4 = 4)

b). – Mzungumzaji ni Bi Farashuu

i. Ametumwa kuonyesha udhalimu wa Bw Makuudi.

ii. Ametumwa kuendeleza maudhui ya uasherati

iii. Ametumwa kuendeleza maudhui ya kisasi

iv. Ametumwa kuendeleza maudhui ya utu

v. Ni kielelezo cha juhudi za wanyonge katika jamii za kupambana na watu wenye uwezo mkubwa.

vi. - Ametumwa kuendeleza maudhui ya utengano. (alama 1 x 8 = 8)

c). Kulingana na maoni ya mzungumzaji, mrejelewa ana dosari. Thibitisha

- Mrejerewa ni Maimuna

i. Maimuna alikuwa amepoteza urembo wake

ii. Alikuwa mkali hapo awali

iii. Alishiriki ukware

iv. Hana asili wale fasili

v. Alikuwa mpenda anasa na starahe.

vi. - Ni mhuni asiyestahili kuolewa. (alama 2 x 4 = 8)

#### SWALI LA 5

Ubabadume – Maana ni taasubi ya kiume, kule kunyanyaswa au kudhalilishwa mkononi mwa wanaume.

i. Mwanamke amekataa kutumiwa kama chombo cha kumstarehesha mwanaume k.m Maimuna kukataa kufanya ngono na James.

ii. Mwanamke, amekataa kutawishwa k.m Maimuna anatoroka nyumbani kwao ili kutafuta uhuru.

iii. Mwanamke anataka awe na usemi na maoni mbele ya mwanaume k.m Biti Kocho kuingilia kati ugomvi kati ya Makuudi na Tamima

iv. Mwanamke anapigania haki ya kupata elimu k.m Maimuna anadai kuwa Serikali itafanya juhudi za kuwaelimisha wasichana

- v. Mwanamke amechoka kutumiwa kama mtumwa k.m Selume kushughulikia familia ilhali mumewe Shoka hashughuliki.
- vi. Mwanamke anapigania kupinga uongozi mbaya unaoendelezwa na wanaume k.m Bi Kazija kuwasuta viongozi wabaya kama Makuudi na Zanga
- vii. Mwanamke kupigania haki ya kumiliki mali k.m Bi Farashuu kulalamika dhidi ya mwanawe Mwanasururu kunyang'anywa mali na Makuudi.
- viii. Mwanamke kudai haki ya kufanya kazi k.m Bi Kazija. (5 x 2 = 10)
- b). Madhara yanayotokana na ubabadume kwa mujibu wa riwaya ya utengano.
- i. Chuki k.m Bi Kazija kuwachukia wanaume Joweri na nafsi yake
- ii. Kulipiza kisasi k.m Kazija , Farashuu na Bi Kocho kuwa na kisasi dhidi ya Makuudi.
- iii. Talaka k.m Makuudi kuwataliki wakeze Tameima na Mwanasururu
- iv. Utumwa k.m Selume kuwachiwa majukumu yote na Bwanake Shoka.
- v. Ujinga k.m Wanawake kama Kazija kufanya kazi na vilevile Mwanasururu kunyang'anywa mali yake.
- vi. Ukwere k.m Wanawake kama Maimuna na Kazija kuonwa kama vyombo vya kuwastarehesha wanaume.
- vii. Kuvunjika kwa familia / ndoa / k.m familia ya Makuudi kusambaratika.
- viii. Umaskini k.m wanawake kama Kazija kutofanya kazi na vilevile Mwanasururu kunyang'anywa mali yake
- ix. Upweke k.m Maimuna na Tamima kutawishwa (5 x 2 = 10)

#### SWALI LA 6

(Kifo kisimani)

a). Mukadha.

- i. Ni maneno ya Mwelusi
- ii. Kwenye uzungumzaji nafsia
- iii. Alikuwa ndani ya gereza.
- iv. - Batu alikuwa amemwacha ili aishawishi akili yake na kufanya uamuzi kuhusu pendekezo la Batu la Mwelusi kujitenga na wachochezi na uchochezi. (1 x 4 = 4)

b). Sifa za msemaji.

Msemaji ni Mwelusi

Sifa:

- (i). Mzalendo
- (ii) Jasiri / Mkakamavu
- (iii). Mtetezi wa haki
- (iv). Mwenye msimamo dhabiti. (alama 2 x1 = 2)

c). Utawala wa mtemi Bokono ni utawala mbaya.

- (i) Kuna uporaji wa mali – Ardhi ya watoto kuchezea kunyakuliwa
- (ii) Utumiaji nguvu – Wananchi wazalendo wa Butangi wanateswa, kutiwa gereza na hata kuuawa ili kuendeleza uongozi mbaya wa Bokono.
- (iii) Umwagikaji wa Damu – Wananchi kuvamiwa na wahuni wa kulipwa, wazalendo kuuawa kikatili (Mwelusi/mtuhumiwa)
- (iv). Kuteswa na kuuawa kwa viongozi wanaodhubutu kutetea haki mf. Kipocha Mwelusi kisimani.
- (v) Kunyimwa haki ya kutumia kisima
- (vi). Njaa na umaskini kukumba wananchi
- (vii) Uharibifu wa mazingira/ Viongozi wanalima popote.
- (viii). Ufisadi na mapendekezo / kumpa mtoto wa Kaloo kazi kwa sababu ni mfuasi/ bonde la Ilangi kunyakuliwa
- (ix). Kutojali kanuni za kulinda ardhi.

(x) Ukosefu wa heshima kwa wanabutangi – Ng'ombe kunywa maji na kuingia kwenye kisima kinachotumiwa na Wanabutangi

(xi). Ukatili – Kuwatumia askari kuwapiga wafungwa, kungoa makucha, kufungwa minyororo

(xii). Unyanyasaji – Mbutwa kutolipwa viti alivyotengeneza kwa mkutano. (7 x 2 = 14)

### FASIHI SIMULIZI

a.(i) Nyiso – Nyimbo zinazoimbwa wakati wavulana wanatiwa jandoni

(ii) Mbolezi – Zinazoimbwa wakati wa matanga

(iii) Hodiya – Nyimbo za kazi

(iv) Bembelezi – Nyimbo zinazoimbiwa watoto wadogo ili kuwabembeleza kulala au kunyamaza wanapolia

(v). Sifo – Nyimbo za sifa, huimbwa kwa malengo ya kuitoa sifa kwa wahusika

b). Hizi ni sherehe au ada za kitamaduni zinazoonyesha usanii wa maonyesho ya kuiga jinsi matukio Fulani yalivyofanyika katika uhalisi wa maisha. (alama 2)

c.(i) Sherehe za mazishi

(ii) Sherehe za kutoa shukurani kwa Mungu baada ya mavuno.

(iii).Nasaha na maadili katika jando na unyago

(iv).Kuomba kabla na baada ya vita.

(v).Sherehe za kuwapa watoto majina baada ya mavuno

(vi) Kutawaza viongozi kwa njia ya kitamaduni

(vii) Kufanya matambiko /kutoa kafara

(viii) Pungo za mapepo. (zozote 1 x 4 = 4)

d. (i) Huleta ubaguzi wa kijinsia kwa kumdhalilisha mwanamke na kumtukuza mwanamme mf. Katika jando, unyago na ndoa.

(ii) Huhifadhi siri za jamii na kuleta utengano baina ya majirani

(iii) Huasi mabadiliko ya kinyakati (sherehe nyingi zimepitwa na wakati)

(iv) .Husababisha kudorora kwa maendeleo

(v). Madhara makubwa hutokea hasa wakati vifaa butu vinapotumiwa kwa shughuli hizo. (zozote 1 x 4 = 4)